

Gal

Chapter 3

Swahili Interlinear

Reference: Swahili Biblica Neno

- 1 Ἐε ἀνόητοι Γαλάται! τίς ὑμᾶς ἐβάσκανεν, <τῆ ἀληθείᾳ μὴ
Ee wajinga Wagalatia nani ninyi aliwaloga kwa-kweli kweli msi
[G5599](#) [G0453](#) [G1052](#) [G5101](#) [G4771](#) [G0940](#) [G3588](#) [G0225](#) [G3361](#)
πείθεσθαι> οἷς κατ' ὀφθαλμοῦς, Ἰησοῦς Χριστὸς προεγράφη
itii ambao-mbele-yenu mbele-ya macho Yesu Kristo alionyeshwa
[G3982](#) [G3739](#) [G2596](#) [G3788](#) [G2424](#) [G5547](#) [G4270](#)
ἐσταυρωμένος?
alisulubiwa
[G4717](#)

Ninyi Wagalatia wajinga! Ni nani aliyewaroga? Yesu Kristo aliwekwa wazi mbele yenu kwamba amesulubiwa.

- 2 τοῦτο μόνον θέλω μαθεῖν ἀφ' ὑμῶν: ἐξ ἔργων νόμου τὸ
hili tu nataka kujifunza kutoka kwenu kwa matendo ya-sheria -huyo
[G3778](#) [G3440](#) [G2309](#) [G3129](#) [G0575](#) [G4771](#) [G1537](#) [G2041](#) [G3551](#) [G3588](#)
Πνεῦμα ἐλάβετε, ἢ ἐξ ἀκοῆς πίστεως?
Roho mlipokea au kwa kusikia kwa-imani
[G4151](#) [G2983](#) [G2228](#) [G1537](#) [G0189](#) [G4102](#)

Nataka nijifunze neno moja kutoka kwenu: Je, mlipokea Roho wa Mungu kwa kushika sheria, au kwa kuyaamini yale mliyosikia?

- 3 οὕτως ἀνόητοί ἐστε? ἐναρξάμενοι Πνεύματι, νῦν σαρκὶ ἐπιτελεῖσθε?
hivyo wajinga ninyi mkianza kwa-Roho sasa kwa-mwili mnamalizia
[G3779](#) [G0453](#) [G1510](#) [G1728](#) [G4151](#) [G3568](#) [G4561](#) [G2005](#)

Je, ninyi ni wajinga kiasi hicho? Baada ya kuanza kwa Roho, je, sasa mwataka kumalizia katika mwili?

- 4 τοσαῦτα ἐπάθετε εἰκῆ? εἶ γε καὶ εἰκῆ?
mengi mlipata bure kama kweli pia bure
[G5118](#) [G3958](#) [G1500](#) [G1487](#) [G1065](#) [G2532](#) [G1500](#)

Je, mlipata mateso kiasi hicho bure? Ni kama kweli yalikuwa bure!

- 5 ὁ οὖν ἐπιχορηγῶν ὑμῖν τὸ Πνεῦμα, καὶ ἐνεργῶν δυνάμεις ἐν
-yule basi anayewapa ninyi -huyo Roho na anayefanya miujiza miongoni
[G3588](#) [G3767](#) [G2023](#) [G4771](#) [G3588](#) [G4151](#) [G2532](#) [G1754](#) [G1411](#) [G1722](#)
ὑμῖν, ἐξ ἔργων νόμου ἢ ἐξ ἀκοῆς πίστεως?
mwenu kwa matendo ya-sheria au kwa kusikia kwa-imani
[G4771](#) [G1537](#) [G2041](#) [G3551](#) [G2228](#) [G1537](#) [G0189](#) [G4102](#)

Je, Mungu huwapa Roho wake na kufanya miujiza katikati yenu kwa sababu mnatii sheria, au kwa sababu mnaamini kile mlichosikia?

6 καθώς Ἄβραάμ ἐπίστευσεν τῷ Θεῷ, καὶ ἐλογίσθη αὐτῷ εἰς
kama-vile Ibrahimu aliamini -huyo Mungu na ilihesabiwa kwake kuwa
[G2531](#) [G0011](#) [G4100](#) [G3588](#) [G2316](#) [G2532](#) [G3049](#) [G0846](#) [G1519](#)

δικαιοσύνην.
haki
[G1343](#)

| Kama vile "Abrahamu alimwamini Mungu na ikahesabiwa kwake kuwa haki."

7 Γινώσκετε ἄρα ὅτι οἱ ἐκ πίστεως, οὗτοι υἱοὶ εἰσιν Ἀβραάμ.
Jueni basi kwamba -wale wa imani hawa wana ni wa-Ibrahimu
[G1097](#) [G0686](#) [G3754](#) [G3588](#) [G1537](#) [G4102](#) [G3778](#) [G5207](#) [G1510](#) [G0011](#)

| Fahamuni basi kwamba wale walio na imani, hao ndio watoto wa Abrahamu.

8 προῖδοῦσα δὲ ἡ γραφή, ὅτι ἐκ πίστεως δικαιοῖ
ikifahamu-mapema basi -hiyo Maandiko kwamba kwa imani huwahesabia-haki
[G4308](#) [G1161](#) [G3588](#) [G1124](#) [G3754](#) [G1537](#) [G4102](#) [G1344](#)

τὰ ἔθνη ὁ Θεὸς, προεσηγγείσατο τῷ Ἀβραάμ ὅτι:
-za mataifa -huyo Mungu yalimhubiri-mapema -huyo Ibrahimu kwamba
[G3588](#) [G1484](#) [G3588](#) [G2316](#) [G4283](#) [G3588](#) [G0011](#) [G3754](#)

Ἐνευλογηθήσονται ἐν σοὶ, πάντα τὰ ἔθνη.
Watabarikiwa katika wewe yote -za mataifa
[G1757](#) [G1722](#) [G4771](#) [G3956](#) [G3588](#) [G1484](#)

| Maandiko yakitabiri kwamba Mungu angewahesabia haki watu wa Mataifa kwa imani, alitangulia kumtangazia Abrahamu Injili akisema kwamba, "Kwa kupitia kwako mataifa yote yatabarikiwa."

9 ὥστε, οἱ ἐκ πίστεως εὐλογοῦνται σὺν τῷ πιστῷ Ἀβραάμ.
hivyo -wale wa imani wanabarikiwa pamoja-na -yule mwaminifu Ibrahimu
[G5620](#) [G3588](#) [G1537](#) [G4102](#) [G2127](#) [G4862](#) [G3588](#) [G4103](#) [G0011](#)

| Kwa sababu hii, wale wote wanaoamini wanabarikiwa pamoja na Abrahamu, mtu wa imani.

10 Ὅσοι γὰρ ἐξ ἔργων νόμου εἰσιν, ὑπὸ κατάραν εἰσίν. γέγραπται
Wote basi wa matendo ya-sheria walio chini-ya laana wako imeandikwa
[G3745](#) [G1063](#) [G1537](#) [G2041](#) [G3551](#) [G1510](#) [G5259](#) [G2671](#) [G1510](#) [G1125](#)

γὰρ ὅτι, Ἐπικατάρατος πᾶς ὃς οὐκ ἐμμένει πᾶσιν τοῖς
basi kwamba Amelaaniwa kila-mtu ambaye ha endelei katika-yote -yale
[G1063](#) [G3754](#) [G1944](#) [G3956](#) [G3739](#) [G3756](#) [G1696](#) [G3956](#) [G3588](#)

γεγραμμένοις ἐν τῷ βιβλίῳ τοῦ νόμου, τοῦ ποιῆσαι αὐτά.
yaliyoandikwa katika -la kitabu cha sheria cha kuyatenda hayo
[G1125](#) [G1722](#) [G3588](#) [G0975](#) [G3588](#) [G3551](#) [G3588](#) [G4160](#) [G0846](#)

| Kwa maana wote wanaotumainia matendo ya sheria wako chini ya laana, kwa kuwa imeandikwa, "Alaaniwe kila mtu asiyeshikilia kutii mambo yote yaliyoandikwa katika Kitabu cha Sheria."

11 ὅτι δὲ ἐν νόμῳ, οὐδεὶς δικαιοῦται παρὰ τῷ Θεῷ, δῆλον;
kwamba basi kwa sheria hakuna anahesabiwa-haki mbele-ya -huyo Mungu ni-wazi
[G3754](#) [G1161](#) [G1722](#) [G3551](#) [G3762](#) [G1344](#) [G3844](#) [G3588](#) [G2316](#) [G1212](#)

ὅτι, Ὁ δίκαιος ἐκ πίστεως ζήσεται.
kwamba Yule mwenye-haki kwa imani ataishi
[G3754](#) [G3588](#) [G1342](#) [G1537](#) [G4102](#) [G2198](#)

| Basi ni dhahiri kwamba hakuna mtu anayehesabiwa haki mbele za Mungu kwa kushikilia sheria, kwa maana, "Mwenye haki ataishi kwa imani."

12 ὁ δὲ νόμος οὐκ ἔστιν ἐκ πίστεως; ἀλλ', Ὁ ποιήσας αὐτὰ ζήσεται
 -hiyo basi sheria si ni ya imani bali Yule atendaye hayo ataishi
[G3588](#) [G1161](#) [G3551](#) [G3756](#) [G1510](#) [G1537](#) [G4102](#) [G0235](#) [G3588](#) [G4160](#) [G0846](#) [G2198](#)
 ἐν αὐτοῖς.
 katika hayo
[G1722](#) [G0846](#)

Lakini sheria haitegemei imani. Kinyume chake, "Mtu atendaye matendo hayo ataishi kwa hayo."

13 Χριστὸς ἡμᾶς ἐξηγόρασεν ἐκ τῆς κατάρας τοῦ νόμου, γενόμενος
 Kristo sisi alitununua kutoka -ile laana ya sheria akiwa
[G5547](#) [G1473](#) [G1805](#) [G1537](#) [G3588](#) [G2671](#) [G3588](#) [G3551](#) [G1096](#)
 ὑπὲρ ἡμῶν κατάρα, ὅτι γέγραπται, Ἐπικατάρατος πᾶς ὁ
 kwa-ajili-yetu yetu laana kwa-sababu imeandikwa Amelaaniwa kila-mtu -yule
[G5228](#) [G1473](#) [G2671](#) [G3754](#) [G1125](#) [G1944](#) [G3956](#) [G3588](#)
 κρεμάμενος ἐπὶ ξύλου;
 aliyening'inia juu-ya mti
[G2910](#) [G1909](#) [G3586](#)

Kristo alitukomboa kutoka laana ya sheria kwa kufanyika laana kwa ajili yetu, kwa maana imeandikwa, "Amelaaniwa yeye aangikwaye juu ya mti."

14 ἵνα εἰς τὰ ἔθνη ἡ εὐλογία τοῦ Ἀβραὰμ γένηται, ἐν Ἰησοῦ
 ili kwa -za mataifa -hiyo baraka ya Ibrahimu ifike katika Yesu
[G2443](#) [G1519](#) [G3588](#) [G1484](#) [G3588](#) [G2129](#) [G3588](#) [G0011](#) [G1096](#) [G1722](#) [G2424](#)
 Χριστῷ, ἵνα τὴν ἐπαγγελίαν τοῦ Πνεύματος λάβωμεν, διὰ τῆς πίστεως.
 Kristo ili -ile ahadi ya Roho tuipokee kwa-njia-ya -ya imani
[G5547](#) [G2443](#) [G3588](#) [G1860](#) [G3588](#) [G4151](#) [G2983](#) [G1223](#) [G3588](#) [G4102](#)

Alitukomboa ili kwamba baraka aliyopewa Abrahamu ipate kuwafikia watu wa Mataifa kwa njia ya Kristo Yesu, ili kwa imani tupate kupokea ile ahadi ya Roho.

15 Ἀδελφοί, κατὰ ἀνθρωπὸν λέγω, ὅμως ἀνθρώπου
 Ndugu kwa-namna-ya-kibinadamu kibinadamu nasema hata ya-mwanadamu
[G0080](#) [G2596](#) [G0444](#) [G3004](#) [G3676](#) [G0444](#)
 κεκυρωμένην διαθήκην, οὐδεὶς ἀθετεῖ, ἢ ἐπιδιατάσσεται.
 iliyothibitishwa agano hakuna anaikataa au anaongeza
[G2964](#) [G1242](#) [G3762](#) [G0114](#) [G2228](#) [G1928](#)

Ndugu zangu, nataka nitoe mfano kutoka maisha ya kila siku. Kama vile hakuna mtu awezaye kutangua au kuongeza kitu katika agano la mtu ambalo limekwisha kuthibitishwa, vivyo hivyo kwa hali kama hii.

16 τῷ δὲ Ἀβραὰμ ἐρρέθησαν αἱ ἐπαγγελίαι, καὶ τῷ σπέρματι αὐτοῦ;
 kwa basi Ibrahimu zilisemwa -hizo ahadi na kwa uzao wake
[G3588](#) [G1161](#) [G0011](#) [G2046](#) [G3588](#) [G1860](#) [G2532](#) [G3588](#) [G4690](#) [G0846](#)
 οὐ λέγει, Καὶ τοῖς σπέρμασιν, ὡς ἐπὶ πολλῶν; ἀλλ' ὡς ἐφ'
 ha yasemi Na kwa-wale mbegu kama juu-ya wengi bali kama juu-ya
[G3756](#) [G3004](#) [G2532](#) [G3588](#) [G4690](#) [G5613](#) [G1909](#) [G4183](#) [G0235](#) [G5613](#) [G1909](#)
 ἑνός, Καὶ τῷ σπέρματί σου, ὃς ἐστὶν Χριστός.
 mmoja Na kwa uzao wako ambaye ni Kristo
[G1520](#) [G2532](#) [G3588](#) [G4690](#) [G4771](#) [G3739](#) [G1510](#) [G5547](#)

Ahadi zilinenwa kwa Abrahamu na kwa mzao wake. Maandiko hayasemi "kwa wazao," likimaanisha watu wengi, bali "kwa mzao wako," yaani mtu mmoja, ndiye Kristo.

17 τοῦτο δὲ λέγω, διαθήκην, προκεκυρωμένην ὑπὸ τοῦ Θεοῦ, ὁ
 hili basi nasema agano lililothibitishwa-kabla na -huyo Mungu -hiyo
[G3778](#) [G1161](#) [G3004](#) [G1242](#) [G4300](#) [G5259](#) [G3588](#) [G2316](#) [G3588](#)

μετὰ τετρακόσια καὶ τριάκοντα ἔτη γεγωνώς, νόμος οὐκ ἄκυροί, εἰς
 baada-ya miaka-mia-nne na thelathini miaka iliyokuja sheria hai batilishi ili
[G3326](#) [G5071](#) [G2532](#) [G5144](#) [G2094](#) [G1096](#) [G3551](#) [G3756](#) [G0208](#) [G1519](#)

τὸ καταργῆσαι τὴν ἐπαγγελίαν.
 -ile kuibatilisha -ile ahadi
[G3588](#) [G2673](#) [G3588](#) [G1860](#)

Ninachotaka kusema ni kwamba, sheria, ambayo ilitolewa miaka 430 baadaye, haitangui Agano lililothibitishwa na Mungu ili kuibatilisha ahadi ile.

18 εἰ γὰρ ἐκ νόμου ἢ κληρονομία, οὐκέτι ἐξ ἐπαγγελίας; τῷ δὲ
 kama basi kwa sheria -hiyo urithi si-tena kwa ahadi kwa basi
[G1487](#) [G1063](#) [G1537](#) [G3551](#) [G3588](#) [G2817](#) [G3765](#) [G1537](#) [G1860](#) [G3588](#) [G1161](#)

Ἄβραᾶμ δι' ἐπαγγελίας, κεχάρισται ὁ Θεός.
 Ibrahimu kwa-njia-ya ahadi alimpa -huyo Mungu
[G0011](#) [G1223](#) [G1860](#) [G5483](#) [G3588](#) [G2316](#)

Kwa maana kama urithi hupatikana kwa sheria, basi hautegemei tena ahadi, lakini Mungu kwa neema yake alimpa Abrahamu urithi kwa njia ya ahadi.

19 Τί οὖν ὁ νόμος? τῶν παραβάσεων χάριν προσετέθη,
 Basi-sheria-ni-nini basi -hiyo sheria ya makosa kwa-sababu-ya iliongezwa
[G5101](#) [G3767](#) [G3588](#) [G3551](#) [G3588](#) [G3847](#) [G5484](#) [G4369](#)

ἄχρις οὗ ἔλθῃ τὸ σπέρμα ᾧ ἐπήγγελται, διαταγείς
 hadi atakapokuja afike -huyo uzao ambaye-kwake aliahidiwa iliyoamriwa
[G0891](#) [G3739](#) [G2064](#) [G3588](#) [G4690](#) [G3739](#) [G1861](#) [G1299](#)

δι' ἀγγέλων ἐν χειρὶ μεσίτου.
 kwa-njia-ya malaika kwa mkono wa-mpatanishi
[G1223](#) [G0032](#) [G1722](#) [G5495](#) [G3316](#)

Kwa nini basi iwepo sheria? Sheria iliwekwa kwa sababu ya makosa mpaka atakapokuja yule Mzao wa Abrahamu, ambaye alitajwa katika ile ahadi. Sheria iliamriwa na malaika kwa mkono wa mpatanishi.

20 ὁ δὲ μεσίτης ἑνὸς οὐκ ἔστιν; ὁ δὲ Θεὸς εἷς ἔστιν.
 -huyo basi mpatanishi wa-mmoja si ni -huyo basi Mungu mmoja ni
[G3588](#) [G1161](#) [G3316](#) [G1520](#) [G3756](#) [G1510](#) [G3588](#) [G1161](#) [G2316](#) [G1520](#) [G1510](#)

Basi mpatanishi huhusisha zaidi ya upande mmoja, lakini Mungu ni mmoja.

21 ὁ οὖν νόμος κατὰ τῶν ἐπαγγελιῶν τοῦ Θεοῦ? μὴ γένοιτο!
 -hiyo basi sheria kinyume-na -za ahadi za Mungu isiwe-hivyo isiwe-hivyo
[G3588](#) [G3767](#) [G3551](#) [G2596](#) [G3588](#) [G1860](#) [G3588](#) [G2316](#) [G3361](#) [G1096](#)

εἰ γὰρ ἐδόθη νόμος ὁ δυνάμενος ζωοποιῆσαι, ὄντως ἐκ νόμου
 kama basi ilitolewa sheria -hiyo yenye-uwezo kutoa-uzima kweli kwa sheria
[G1487](#) [G1063](#) [G1325](#) [G3551](#) [G3588](#) [G1410](#) [G2227](#) [G3689](#) [G1537](#) [G3551](#)

ἂν ἦν ἡ δικαιοσύνη;
 ingekuwa ingekuwa -hiyo haki
[G0302](#) [G1510](#) [G3588](#) [G1343](#)

Je basi, sheria inapingana na ahadi za Mungu? La hashu! Kwa maana kama sheria iliyotolewa ingeweza kuwapa watu uzima, basi haki ingepatikana kwa njia ya sheria.

22 ἀλλὰ συνέκλεισεν ἢ γραφὴ τὰ πάντα ὑπὸ ἁμαρτίαν, ἵνα ἢ
lakini zilifunga -hizo Maandiko -za vitu-vyote chini-ya dhambi ili -hiyo
[G0235](#) [G4788](#) [G3588](#) [G1124](#) [G3588](#) [G3956](#) [G5259](#) [G0266](#) [G2443](#) [G3588](#)

ἐπαγγελία, ἐκ πίστεως Ἰησοῦ Χριστοῦ, δοθῆ τοῖς πιστεύουσιν.
ahadi kwa imani ya-Yesu Kristo itolewe kwa-wale wanaoamini
[G1860](#) [G1537](#) [G4102](#) [G2424](#) [G5547](#) [G1325](#) [G3588](#) [G4100](#)

Lakini Maandiko yamefanya vitu vyote vifungwe chini ya nguvu ya dhambi, ili yale yaliyoahidiwa kwa njia ya imani katika Yesu Kristo yapate kupewa wale wanaoamini.

23 Πρὸ τοῦ δὲ ἐλθεῖν τὴν πίστιν, ὑπὸ νόμον ἐφρουρούμεθα,
Kabla ya basi kuja -hiyo imani chini-ya sheria tulilindwa
[G4253](#) [G3588](#) [G1161](#) [G2064](#) [G3588](#) [G4102](#) [G5259](#) [G3551](#) [G5432](#)

συνκλειόμενοι εἰς τὴν μέλλουσαν πίστιν ἀποκαλυφθῆναι.
tukifungwa hadi -ile itakayokuja imani ifunuliwe
[G4788](#) [G1519](#) [G3588](#) [G3195](#) [G4102](#) [G0601](#)

Kabla imani hii haijaja tulikuwa tumewekwa chini ya sheria, tumefungwa mpaka ile imani ifunuliwe.

24 ὥστε ὁ νόμος, παιδαγωγὸς ἡμῶν γέγονεν, εἰς Χριστόν, ἵνα ἐκ πίστεως
hivyo -hiyo sheria mlezi wetu ilikuwa hadi Kristo ili kwa imani
[G5620](#) [G3588](#) [G3551](#) [G3807](#) [G1473](#) [G1096](#) [G1519](#) [G5547](#) [G2443](#) [G1537](#) [G4102](#)

δικαιωθῶμεν.
tuhesabiwe-haki
[G1344](#)

Hivyo, sheria ilikuwa kiongozi kutufikisha kwa Kristo, ili tupate kuhesabiwa haki kwa imani.

25 ἐλθούσης δὲ τῆς πίστεως, οὐκέτι ὑπὸ παιδαγωγόν ἐσμεν;
baada-ya-kuja basi -ile imani si-tena chini-ya mlezi tuko
[G2064](#) [G1161](#) [G3588](#) [G4102](#) [G3765](#) [G5259](#) [G3807](#) [G1510](#)

Lakini sasa kwa kuwa ile imani imekuja, hatuimamiwi tena na sheria.

26 Πάντες γὰρ υἱοὶ Θεοῦ ἐστε, διὰ τῆς πίστεως ἐν Χριστῷ
Ninyi-nyote basi wana wa-Mungu ninyi kwa-njia-ya -ya imani katika Kristo
[G3956](#) [G1063](#) [G5207](#) [G2316](#) [G1510](#) [G1223](#) [G3588](#) [G4102](#) [G1722](#) [G5547](#)

Ἰησοῦ.
Yesu
[G2424](#)

Kwa maana ninyi nyote mmekuwa watoto wa Mungu katika Kristo Yesu kwa njia ya imani.

27 ὅσοι γὰρ εἰς Χριστόν ἐβαπτίσθητε, Χριστόν ἐνεδύσασθε.
wote basi katika Kristo mliobatizwa Kristo mmemvaa
[G3745](#) [G1063](#) [G1519](#) [G5547](#) [G0907](#) [G5547](#) [G1746](#)

Kwa maana wote mliobatizwa ndani ya Kristo, mmemvaa Kristo.

28 οὐκ ἔνι Ἰουδαῖος οὐδὲ Ἕλληνας; οὐκ ἔνι δοῦλος οὐδὲ ἐλεύθερος;
hakuna tena Myahudi wala Mgiriki hakuna tena mtumwa wala huru
[G3756](#) [G1762](#) [G2453](#) [G3761](#) [G1672](#) [G3756](#) [G1762](#) [G1401](#) [G3761](#) [G1658](#)

οὐκ ἔνι ἄρσεν καὶ θῆλυ; πάντες γὰρ ὑμεῖς εἶς ἐστε, ἐν
hakuna tena mwanaume na mwanamke ninyi-wote basi ninyi mmoja ninyi katika
[G3756](#) [G1762](#) [G0730](#) [G2532](#) [G2338](#) [G3956](#) [G1063](#) [G4771](#) [G1520](#) [G1510](#) [G1722](#)

Χριστῷ Ἰησοῦ.
Kristo Yesu
[G5547](#) [G2424](#)

| Wala hakuna tena Myahudi au Myunani, mtumwa au mtu huru, mwanaume wala mwanamke, maana nyote mmekuwa wamoja ndani ya Kristo Yesu.

29 εἰ δὲ ὑμεῖς Χριστοῦ, ἄρα τοῦ Ἀβραάμ σπέρμα ἐστέ, κατ'
kama basi ninyi wa-Kristo basi wa Ibrahimu uzao ninyi kwa-mujibu-wa
[G1487](#) [G1161](#) [G4771](#) [G5547](#) [G0686](#) [G3588](#) [G0011](#) [G4690](#) [G1510](#) [G2596](#)

ἐπαγγελίαν κληρονόμοι.
ahadi warithi
[G1860](#) [G2818](#)

| Nanyi mkiwa ni mali ya Kristo, basi ninyi ni wa uzao wa Abrahamu na warithi sawasawa na ile ahadi.